# ANDIKO LA MRADI

## TAMASHA LA KIMATAIFA LA HISTORIA LA JULIUS KAMBARAGE NYERERE – 2026

### JUKANYE INTERNATIONAL HISTORY FESTIVAL – 2026

**Waandaaji:**

JASIRI ARTS & CULTURE INSTITUTION (JACI)
**Usajili:** Chini ya Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA)
CATZ COMPANY LIMITED
**Usajili:** BRELA - **173701225**

**Mlezi wa Tamasha:** Bi. Anna Julius Nyerere


JASIRI ARTS & CULTURE INSTITUTION (JACI)
S.L.P 38012, Dar es Salaam, Tanzania
Simu: 0789 388232 / 0673 023547
Email: jukanyefestival@gmail.com

CATZ COMPANY LIMITED
**S.L.P 196601, Dar Es Salaam Tanzania,**
**Simu: +255 746 174403 / +255 673196681**
**Email: catzcom2024@gmail.com**

**YALIYOMO** **UKURASA**


| | |
|---|---|
| **Utangulizi, Vyanzo vya Mapato, Faida za Kiuchumi** | **2 - 3** |
| **Tuzo ……………………………………………….…..** | **4** |
| **Madaraja ya Wadhamini……………………………...** | **10** |
| **Mwisho ………………………………………………………** | **11** |

## UTANGULIZI

## TAMASHA LA KIMATAIFA LA HISTORIA LA JULIUS KAMBARAGE NYERERE (JUKANYE) – JULIUS KAMBARAGE NYERERE INTERNATIONAL HISTORY FESTIVAL (JUKANYE)

**Taasisi ya JASIRI ARTS & CULTURE (JACI) kwa kushirikiana na CATZ COMPANY LIMITED** inatangaza maandalizi ya Tamasha la Kimataifa la Historia la JUKANYE2026, tukio la kila baada ya miaka miwili linaloenzi urithi wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

**Kaulimbiu:** "Uchumi wa Afrika Utaimarishwa na Waafrika Kupitia Umoja"
**Lengo Kuu:** Kuenzi viongozi wa Afrika waliopigania uhuru na kuhamasisha uzalendo kwa kizazi cha sasa.
**Dhima na Maono:** Kuwa jukwaa la kuenzi historia ya ukombozi wa Afrika kupitia mchango wa viongozi wake, hasa wakiongozwa na Mwalimu Nyerere, kupitia utalii, sanaa, makongamano, maonesho, na burudani za kitamaduni.
**Urithi wa Mwalimu Nyerere:** Kuendeleza maono na misingi ya mshikamano, utu, amani, ukweli, unyenyekevu, na upendo kwa watu wake; kuhakikisha fikra na maadili haya yanatunzwa kwa vizazi vijavyo.

### Mahali na Tarehe

- **Mkoa:** Arusha, Tanzania
- **Ufunguzi:** Jumanne, 1 Septemba 2026
- **Kufunga:** Jumapili, 13 Septemba 2026 (Utoaji wa Tuzo)
- **Muda:** Siku 13 (Maonyesho, Utalii, Warsha, Huduma za Kijamii, Tuzo)

### Malengo Mahsusi

1. Kuhifadhi historia ya ukombozi na kuelimisha vizazi.
2. Kukuza uchumi, ubunifu, ajira, na ushiriki wa vijana.
3. Kuimarisha uzalendo, amani, mshikamano, na haki za kijamii.
4. Kutangaza Kiswahili, utamaduni, na urithi wa Afrika.
5. Kulinda mazingira na kuendeleza maono ya Mwalimu Nyerere kwa umoja na maendeleo.

### Vipengele vya Tamasha

- Maonyesho ya makumbusho ya viongozi wa Afrika na mchango wao.
- Burudani za muziki wa asili na kisasa kutoka mataifa mbalimbali.
- Michezo ya kuigiza historia ya ukombozi.
- Maonyesho ya mavazi na utamaduni wa nchi washiriki.
- Makongamano kwa vijana na wadau kujadili maendeleo ya Afrika.
- Kliniki za afya kwa jamii.
- Ziara za kihistoria na kitalii (Butiama, Tabora, Dar es Salaam, Zanzibar, na mikoa ya Kusini).
- Kuendeleza matumizi ya nishati salama za kupikia.
- Uzinduzi wa makala maalum kuhusu Mwalimu Nyerere.
- Madarasa ya Kiswahili kwa wageni.
- **Utoaji wa tuzo kwa viongozi vinara wa ukombozi wa Afrika, Tuzo ya Mama Afrika kwa baadhi ya wake wa viongozi wapigania uhuru na wanawake wanaharakati wa ukombozi, Tuzo ya Sauti za Hekima kwa Viongozi waliotumia imani (ushawishi wa kiroho) katika kuchochea harakati za kumkomboa mwafrika, Tuzo za Mshikamano kwa mataifa ya nje ya Africa yalioliunga mkono bara la Afrika kwenye harakati zake za ukombozi, Tuzo za**

**heshima kwa Baadhi ya marais wa sasa wazalendo kwa bara la Afrika na Tuzo za muziki wa ukombozi kwa wanamuziki waliotumia tungo zao kuchochea harakati za ukombozi barani Afrika.**

**Viongozi Wakuu Wanaotarajiwa Kualikwa**

- **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan** – Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Mgeni Rasmi wa Ufunguzi)
- **Mhe. Miguel Díaz-Canel** – kwa niaba ya UNESCO (Mgeni Rasmi wa Utoaji wa Tuzo za Heshima)
- **Kapteni Ibrahim Traoré** – Rais wa Mpito wa Burkina Faso (Mgeni wa Kufunga Tamasha)

**Washiriki:** Nchi zote za Afrika, mataifa rafiki, wadau wa kimataifa, mashirika ya elimu, maendeleo, na utamaduni.

**Bajeti na Mapato**

- Bajeti ya tamasha: takriban **Shilingi Bilioni 3.4** (maandalizi, usafiri, teknolojia, usalama, tuzo, matangazo).
- Mapato yatatumika kugharamia maandalizi yote, malipo ya watendaji na wasanii, malazi, chakula, uzalishaji wa makala rasmi, kuendeleza tamasha lijalo, kusaidia vijana, na kuimarisha makumbusho ya taifa kwa kuiweka katika katika mfumo wa kigitali (Digitization of the national Museum sites and monuments).

**Vyanzo vya Mapato:**

1. Wadhamini na wafadhili (Platinum, Gold, Silver, Bronze)
2. Michango ya nchi zinazonufaika
3. Michango ya wadau binafsi na taasisi
4. Uuzaji wa mahema ya maonyesho
5. Bidhaa rasmi za tamasha (vitabu, vitambaa, mashati, kofia, nk.)

**Faida kwa Wadhamini:** Utambulisho wa kitaifa na kimataifa, nembo kwenye jukwaa, fulana, mabango, mitandao ya kijamii, nafasi za biashara, mialiko maalum.

**Faida za Kiuchumi kwa Tanzania**

- **Muda Mfupi:** Kuongezeka kwa mapato sekta za malazi, usafiri, chakula; ajira za muda mfupi; uuzaji wa bidhaa za mikono; kodi na tozo zaidi kwa serikali.
- **Muda Mrefu:** Kukuza utalii wa kihistoria na kiutamaduni; kuvutia uwekezaji; kuimarisha utambulisho wa Tanzania kimataifa; kuendeleza vipaji vya vijana na uchumi wa ubunifu.

**Maeneo Yanayotarajiwa:** Butiama, Dar es Salaam, Zanzibar, Tabora, Kilimanjaro, Arusha, Manyara, mikoa ya Kusini, na mikoa mingine itakayoshiriki.

**Wito Rasmi kwa:** Serikali, wizara husika, mashirika, makampuni, wadau wa ndani na nje, mashirika ya kimataifa, sekta binafsi na biashara.

**TUZO**


**VIONGOZI MASHUHURI WATAKAOPATA TUZO**


Orodha ya viongozi mashuhuri wa Africa waliopigania uhuru, tuanatarajia kutoa tuzo za heshima katika Tamasha la JUKANYE INTERNATIONAL HISTORY FESTIVAL – 2026;

| | NCHI | KIONGOZI | HALI |
|---|---|---|---|
| 1 | Tanzania | Mwalimu Julius Kambarage Nyerere | Marehemu |
| 2 | Zanzibar | Abeid Amani Karume | Marehemu |
| 3 | Kenya | Jomo Kenyatta | Marehemu |
| 4 | Uganda | Milton Obote | Marehemu |
| 5 | Ghana | Kwame Nkrumah | Marehemu |
| 6 | Afrika Kusini | Nelson Mandela | Marehemu |
| 7 | Zimbabwe | Robert Mugabe | Marehemu |
| 8 | Algeria | Ahmed Ben Bella | Marehemu |
| 9 | Guinea | Ahmed Sékou Touré | Marehemu |
| 10 | Angola | Agostinho Neto | Marehemu |
| 11 | Namibia | Sam Nujoma | Hai |
| 12 | Msumbiji | Samora Machel | Marehemu |
| 13 | Zambia | Kenneth Kaunda | Marehemu |
| 14 | Malawi | Hastings Kamuzu Banda | Marehemu |
| 15 | Ethiopia | Haile Selassie | Marehemu |
| 16 | Burkina Faso | Thomas Sankara | Marehemu |
| 17 | Libya | Muammar Gaddafi | Marehemu |
| 18 | Nigeria | Nnamdi Azikiwe | Marehemu |
| 19 | Senegal | Léopold Sédar Senghor | Marehemu |
| 20 | Cameroon | Ahmadou Ahidjo | Marehemu |
| 21 | Congo (DRC) | Patrice Lumumba | Marehemu |

# AFRICAN LIBERATION FIGHTERS TO BE HONORED AND AWARDED AT THE JUKANYE INTERNATIONAL HISTORY FESTIVAL – 2026



Mwalimu Julius Kambarage Nyerere


Abeid Amani Karume - Zanzibar



Mzee Jomo Kenyatta - Kenya


Milton Obote - Uganda


Nelson Mandela - Afrika Kusini


Kwame Nkrumah - Ghana


Robert Mugaba - Zimbabwe


Ahmed Ben Bella - Algeria


Ahmed Sékou Touré - Guinea


Agostinho Neto - Angola



Sam Nujoma - Namibia


Samora Machel - Msumbiji


Kenneth Kaunda - Zambia


Congo (DRC) - Ghana


Hastings Kamuzu Banda - Malawi


Nnamdi Azikiwe -- Nigeria


Thomas Sankara - Burkina Faso


Muammar Gaddafi - Libya


Emperor HaileSelassie_I - Ethiopia


Léopold Sédar Senghor - Senegal


Ahmadou Ahidjo - Cameroon




In honor of your unwavering courage and visionary leadership that ignited the flame of Africa's freedom."
"Your legacy of sacrifice and liberation shall forever shine as a beacon for generations to come.

Kwa heshima ya ujasiri wako usiotetereka na uongozi wa maono uliochochea mwanga wa uhuru wa Afrika."
"Urithi wako wa kujitolea na ukombozi utaendelea kung'ara sasa na mpaka vizazi vijavyo."

**TUZO YA MAMA AFRIKA KWA UKOMBOZI NA URITHI"**
**(Mama Afrika Award For Liberation And Legacy)**

Tunaheshimu na kutambua mchango mkubwa wa wanawake wanaharakati na wake wa viongozi waliopigania uhuru wa Afrika. Tamasha la **JUKANYE INTERNATIONAL HISTORY FESTIVAL – 2026** litatoa tuzo za heshima kwa wanawake hawa wa mfano, kwa jitihada zao zisizopimika katika harakati za ukombozi wa bara letu.

| | NCHI | KIONGOZI | HALI |
|---|---|---|---|
| 1 | Afrika Kusini | **Winnie Madikizela-Mandela** | Marehemu |
| 2 | Nigeria | **Funmilayo Ransome-Kuti** | Marehemu |
| 3 | Tanzania | **Maria Nyerere** | Hai |
| 4 | Msumbiji | **Josina Machel** | Marehemu |
| 5 | Msumbiji | **Graça Machel** | Hai |
| 6 | Angola | **Queen Nzinga** – *(Karne ya 17)* | Marehemu |
| 7 | Kenya | **Mama Ngina Kenyatta** | |
| 8 | Tanzania | **Bibi Titi Mohamed** | Marehemu |




## TUZO YA HEKIMA YA UKOMBOZI – WISDOM OF LIBERATION AWARD

Tuzo hii itatolewa kwa viongozi wa kidini waliotoa mchango mkubwa katika harakati za ukombozi wa Afrika kwa kutumia maadili, imani, na ushawishi wao kuhamasisha mapambano dhidi ya ukoloni, udhalimu, na utumwa wa kiakili barani Afrika. Tuanatarajia kutoa tuzo hii kwa:

| | NCHI | KIONGOZI | HALI |
|---|---|---|---|
| 1 | Afrika Kusini | **Archbishop Desmond Tutu** | Marehemu |
| 2 | Ethiopia | **Abuna Theophilos** | Marehemu |
| 3 | Zimbabwe | **Bishop Abel Muzorewa** | Marehemu |


HEKIMA YA UKOMBOZI



Archbishop Desmond Tutu- Afrika Kusini



Abuna Theophilos - Ethiopia



Bishop Abel Muzorewa - Zimbabwe

---

## TUZO MAALUMU ZA HESHIMA

Tuzo hizi zitatolewa kwa baadhi ya viongozi wa Afrika wa sasa, kama ishara ya kutambua na kuenzi mchango wao mkubwa katika kuleta maendeleo, kukuza umoja, na uzalendo katika bara letu. Tuanatarajia kutoa tuzo hizi kwa:

| | NCHI | KIONGOZI | HALI |
|---|---|---|---|
| 1 | Tanzania | **Dr. Samia Suluhu Hassan** | Rais |
| 2 | Uganda | **Yoweri Kaguta Museven** | Rais |
| 3 | Rwanda | **Paul Kagame** | Rais |
| 4 | Burkina Faso | **Ibrahim Traoré** | Rais |
| **5** | Benin | **Patrice Talon** | Rais |



Rais Dr. Samia Suluhu Hassan - Tanzania



Rais Paul Kagame - Rwanda



Rais Captain Ibrahim Traoré - Burkina Faso



Rais Patrice talon - Benin



Rais Yoweri Kaguta Museveni - Uganda

TUZO YA MSHIKAMANO (Solidarity Award)

**Tuanatarajia kutoa tuzo kwa nchi za nje ya Africa zilizosaidia katika ukombozi barani Afrika.**

Tunatarajia kutoa tuzo hizi kwa nchi zifuatazo;

- China
- Urusi
- Cuba




---

TUZO YA SAUTI YA UKOMBOZI WA AFRIKA (MUZIKI)

Tuzo hizi zimegawanywa katika makundi matatu, na mshindi mmoja atachaguliwa kutoka kila kundi kupitia kura za mtandaoni kwenye Tovuti na App ya JUKANYE. Kila mshindi atapokea tuzo pamoja na fedha taslimu kulingana na kundi lake.

A. KUNDI LA WANAMUZIKI WA NJE YA AFRIKA - ZAMANI

| | NCHI | Msanii | HALI | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Jamaica | Bob Marley | Marehemu | 2 |
| 2 | Jamaica | Peter Tosh | Marehemu | |
| 3 | Jamaica | Culture - Joseph Hill | Marehemu | |
| 4 | Jamaica | Burning Spear - Winstone Rodney | Hai | |
| 5 | Marekani | Harry Belafonte | Marehemu | |
| 6 | Jamaica | Rita Marley | Hai | |
| 7 | Guyana | Eddy Grant | Hai | |
| | | | | **2** |

B. KUNDI LA WANAMUZIKI WA NJE YA AFRIKA - SASA

| | NCHI | Msanii | HALI | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Senegal | Youssou N'Dour | Hai | 1 |
| 2 | Haiti/USA | Wyclef Jean | Hai | |
| | | | | **1** |

C. KUNDI LA WANAMUZIKI WA AFRIKA - ZAMANI

| | NCHI | Msanii | HALI | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Afrika Kusini | Miriam Makeba | Marehemu | 1 |
| 2 | Afrika Kusini | Hugh Masekela | Marehemu | |
| 3 | Zimbabwe | Thomas Mapfumo | Hai | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 4 | Nigeria | Fela Kuti | Marehemu | |
| | | | | **2** |

D. KUNDI LA WANAMUZIKI WA AFRIKA - SASA

| | NCHI | Msanii | HALI | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Ivory Coast | Tiken Jah Fakoly | Hai | 2 |
| 2 | Ghana | Rocky Dawuni | Hai | |
| 3 | Ivory Coast | Alpha Blondy | Hai | |
| 4 | Afrika Kusini | Lucky Dube | Marehemu | |
| 5 | Afrika Kusini | Yvonne Chaka Chaka | Hai | |
| 6 | Afrika Kusini | Ladysmith Black Mambazo | Hai | |
| 7 | Zimbabwe | Oliver Mtukudzi | Marehemu | |
| 8 | Tanzania | Dkt. Remmy Ongala | Marehemu | |
| 9 | Tanzania | Hamza Kalala | Hai | |
| | | | | **2** |

E. KUNDI LA WANAMUZIKI WA TANZANIA - ZAMANI

| | MJI | Msanii | HALI | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Kigoma/Dsm | Marijani Rajab (Tanzania) | Marehemu | **2** |
| 2 | Dsm | Western Jazz Band (Tanzania) | Marehemu | |
| 3 | Tanga | Steven John Hiza (Tanzania) | Hai | |
| 4 | Morogoro | Mbaraka Mwinshehe | Marehemu | |
| 5 | Katavi | Hamza Kalala | Hai | |
| 6 | Zanzibar | Bi Kidude | Marehemu | |
| | | | | **2** |

F. KUNDI LA WANAMUZIKI WA TANZANIA - SASA

| | MJI | Msanii | HALI | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | DSM | Jhikoman (Jhikolabwino) | Hai | 2 |
| 2 | DSM | Captain John Komba | Marehemu | |
| 3 | DSM | Msafiri Zawose | Hai | |
| 4 | DSM | Khadija Kopa | Hai | |
| 5 | DSM | Vick Kamata | Hai | |
| | | | | **2** |

| | |
|---|---|
| **JULA TUZO:** | **51** |

**MADARAJA YA WADHAMINI (SPONSORSHIP TIERS) KWA BAJETI YA (TZS 3.4 Bilioni)**

| Daraja | Kiasi (TZS) | Kiasi (%) | Faida Muhimu (Muhtasari) |
|---|---|---|---|
| **Platinum** | 1,500,000,000 | 44% | Nembo kubwa jukwaani, matangazo ya kipekee, hotuba uzinduzi, nafasi za tuzo, meza maalumu, matangazo TV/Redio |
| **Gold** | 1,000,000,000 | 29% | Hotuba uzinduzi, kupamba maeneo ya semina, matangazo, nafasi za tuzo, meza maalumu, banda la maonyesho |
| **Silver** | 600,000,000 | 18% | Matangazo TV/Redio, meza maalumu, banda la maonyesho, tuzo, mavazi ya mdhamini |
| **Bronze** | 250,000,000 | 7% | Banda la maonyesho, kutajwa kwenye mabango na kumbukumbu, tuzo, mavazi ya mdhamini |
| **Wachangiaji Marafiki** | Kuanzia 50,000 | — | Kutajwa kwenye kumbukumbu za marafiki wa tamasha, mshikamano wa kijamii, taarifa maalumu na shukrani |

---

**Muhtasari wa Gharama**

- **Jumla:** TZS 3,350,000,000 (Wadhamini wakuu) + Michango ya Marafiki
- Wachangiaji marafiki hutoa michango kuanzia TZS 50,000, ikisaidia kutekeleza vipengele vya tamasha na kushiriki kama wafuasi wa tukio.
- Wadhamini wakubwa hupata huduma na ushawishi wa kipekee, wachangiaji marafiki wanathaminiwa kwa mchango wa mshikamano.

---

Wachangiaji Marafiki wa Jukanye

Tunawakaribisha watu binafsi, makundi, na taasisi kuchangia kwa moyo wote katika Tamasha la JUKANYE INTERNATIONAL HISTORY FESTIVAL – 2026 kama **Wachangiaji Marafiki wa Jukanye**.

Michango ya Wachangiaji Marafiki inaweza kuanzia **shilingi 50,000 (ELFU HAMSINI)** na zaidi, bila kikomo cha juu, na kila mchango utasaidia moja kwa moja kufanikisha maandalizi na utekelezaji wa tamasha hili muhimu.

**Faida za kuwa Mchangiaji Marafiki:**

- Kutajwa rasmi katika kumbukumbu za tamasha kama marafiki wa tukio
- Kupokea taarifa maalumu za maendeleo ya tamasha
- Kushiriki katika mshikamano wa kijamii unaoleta maendeleo ya Afrika kupitia urithi wa Mwalimu Nyerere.
- Fursa ya kushiriki katika hafla za tamasha kama washirika wa heshima.(Vigezo na maharti kuzingatiwa)

***Tunathamini kila mchango unaoleta usaidizi na mshikamano wa pamoja. Jiunge nasi, tuendeleze urithi wa ukombozi wa Afrika pamoja!***

WASILIANA NASI KWA:

1. Kudhamini, Kufadhiri, kusaidia kwa hari, mali na ushauri
2. Kushiriki , kukodi Vizimba vya maonyesho ama kutoa huduma nyingine katika maonesho
3. Kununua Bidhaa za Tamasha

---

***HITIMISHO:***

*JUKANYE INTERNATIONAL HISTORY FESTIVAL – 2026 ni dira ya kurithisha historia, kulinda utambulisho wa Mwafrika, kukuza ushirikiano wa bara letu, na kuitangaza Tanzania kama nguzo ya maendeleo ya ki-Afrika. Tunakaribisha ushirikiano wa dhati kutoka kwa serikali, mashirika, taasisi, vyuo vikuu, taasisi za kifedha na watu binafsi katika kufanikisha tukio hili la kihistoria.*

**Kwa Taarifa Zaidi Tembelea [https://www.jukanye.com](https://www.jukanye.com) Ama Tuandikie info@jukanye.com**


JASIRI ARTS & CULTURE INSTITUTION (JACI)
S.L.P 38012, Dar es Salaam, Tanzania
Simu: 0789 388232 / 0673 023547
Email: jukanyefestival@gmail.com

CATZ COMPANY LIMITED
**S.L.P 196601, Dar Es Salaam Tanzania,**
**Simu: +255 746 174403 / +255 673196681**
**Email: catzcom2024@gmail.com**


---


**Imeandaliwa na:**
**CATZ COMPANY LIMITED**
**+255 746 174403, [yetuapp@gmail.com](mailto:yetuapp@gmail.com)**